# Riwaya ya Kiswahili kama Tahakiki ya Jamii Baada-ukoloni

*Mwenda Mbatiah*

*Ikisiri*

Makala haya yanachukulia kwamba mwandishi wa Kiswahili haandiki tu kwa ajili ya kuandika bali huandika kukidhi mahitaji ya jamii anayoiandikia. Makala yanarejelea jamii pana ya Afrika Mashariki inayotumia lugha ya Kiswahili. Jamii ya mwandishi pia inaweza kuwa nchi mojawapo ya Afrika Mashariki. Tunatambua kwamba fasihi ya Kiswahili ina hadhira pana zaidi kwa maana ya kuwa inaweza kusomwa mahali popote ulimwenguni. Hata hivyo, mwandishi wa Kiswahili huilenga kwanza jamii yake. Hili ni jambo ambalo waandishi wengi wamekiri. Euphrase Kezilahabi, kwa mfano, amesema kwamba huwaandikia Watanzania, hasa wakulima wa mashambani.[i] Njia mojawapo ya mwandishi kutimiza matarajio ya jamii anayoiandikia ni kumulika kiini cha matatizo na uozo wa jamii inayohusika. Mwandishi hujaribu kujibu maswali kama vile: Kwa nini Mwafrika anatupa utamaduni wake na kuabudu Uzungu? Kwa nini mataifa huru ya Kiafrika hayawezi kujitegemea kiuchumi? Kwa nini maovu kama dhuluma, ufisadi na utawala mbaya yanazidi kuenea? Jawabu la maswali haya na mengine mengi, linahusiana na historia yetu, hasa kutawaliwa kikoloni. Waandishi wengi wa riwaya ya Kiswahili wanashughulikia athari hizi za ukoloni katika jamii zao. Hili ndilo suala ambalo makala haya yanajadili kwa kutumia data ya riwaya nne.

## 1.0 Utangulizi

Tangu chimbuko lake katika enzi ya Shaaban Robert riwaya ya Kiswahili imedumisha mkondo wa kimaudhui ambao unaelezeka kama uhakiki wa jamii za Afrika Mashariki. Watunzi wa riwaya katika enzi mbalimbali tangu miaka ya 1960 mpaka leo wameendelea kumulika masuala makuu yaliyokuwa na athari kubwa kwa walio wengi katika jamii husika. Tukio kuu la kihistoria lililozua mataifa ya kisasa ya Afrika Mashariki ni majilio ya ukoloni. Wakoloni ndio waliojikatia vipande mbalimbali ya bara la Afrika ambavyo baadaye vilikuja kuwa mataifa ya Kiafrika yaliyoanza kupata uhuru wa kisiasa katika miaka ya 1960. Lengo la wakoloni katika kuyabuni mataifa haya lilikuwa ni kustawisha uchumi wa nchi zao kwa kutumia maliasili kama vile ardhi na madini katika makoloni yao. Lengo kama hili halingeweza kutimizwa bila kuwatawala kimabavu wenyeji, kuangamiza tamaduni zao na kuwanyang'anya mali. Matatizo ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni ambayo waandishi wa riwaya ya Kiswahili wanayajadili katika kazi zao yanahusiana na historia hii ya ukoloni. Lengo kuu la makala haya ni kuchunguza vipengele vikuu vya taswira ya jamii baada-ukoloni inayosawiriwa na watunzi wa riwaya na kutathmini mawazo yao kuvihusu.[ii] Tunachukulia kwamba waandishi wa riwaya hawatoi tu picha ya jamii zinazohusika bali wanazihakiki, wanabainisha matatizo yanayozikumba jamii hizi na kuangazia chanzo chake.

Japokuwa mada yetu inahusu mkondo mkuu wa kimaudhui wa riwaya ya Kiswahili kwa ujumla, tumeteua riwaya nne ambazo tunazirejelea katika mjadala wetu. Riwaya hizi ni zifuatazo: *Utubora Mkulima* (1968) ya Shaaban Robert, *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) ya Euphrase Kezilahabi, *Mwisho wa Kosa* (1987) ya Zainabu Burhani na *Walenisi* (1995) ya Katama Mkangi. Riwaya hizi zimeteuliwa kwa sababu zinawakilisha miongo minne ya uandishi wa riwaya ya Kiswahili tangu chimbuko lake. Pili, riwaya hizi ni tungo pevu ambazo zinaweza kuchukuliwa kama vielelezo vya uandishi bora wa riwaya ya Kiswahili.

Utaratibu tunaoutumia katika kushughulikia mada hii ni kuchanganua vipengele vikuu vya taswira za jamii za Afrika Mashariki ambazo zinasawiriwa na waandishi wanaohusika. Vipengele hivi ni dola na utamaduni. Tunathibitisha kwamba vipengele hivi viwili vina upana mkubwa na vitanzu vingi.

## 2.0 Dola

Kwa kiwango kikubwa, dola zinazosawiriwa katika riwaya zilizotajwa hapo juu ni zile za mataifa huru ya Afrika Mashariki. Hii ina maana kwamba dola ya kikoloni, yaani kabla ya uhuru imerejelewa kwa kiasi kidogo sana. Hata hivyo, tunadokezewa hali ya dola ya kikoloni katika riwaya ya *Utubora Mkulima*. Mwanzoni mwa riwaya hii tunaelezwa kwamba Utubora anakatiziwa mpango wa kufunga ndoa ili aitikie mwito wa serikali ya Kiingereza wa kwenda vitani (uk. 10). Vita vinavyorejelewa hapa ni Vita Vikuu vya Pili vya Dunia. Hivi ni vita ambavyo vilihusu zaidi mataifa ya Ulaya kama vile Uingereza na Ujerumani. Uingereza iliwashurutisha raia wa makoloni yake kujiunga na jeshi lake na kwenda kupigana katika sehemu mbalimbali za dunia. Utubora anaingia jeshini na kwenda kupigana huko Burma. Kama tunavyofahamu kutokana na historia, vita hivi vilisababisha maangamizi makubwa ya mali na maisha. Katika riwaya tunaona jinsi Bimkubwa anavyoathirika na maisha yake kugubikwa na upweke baada ya kumpoteza mjukuu wake anayeangamia vitani. Kwa upande wake, Utubora anaathirika kwa njia mbalimbali. Japokuwa ananusurika na kurudi nyumbani baada ya vita, anakuta mchumba wake alishaolewa na mtu mwingine. Pili, anakuta mamake akiwa ameshafariki. Mapigo haya makubwa yanabadilisha maisha yake.

Kitendo cha Uingereza kuwachukua vijana wa Kiafrika na kuwapeleka kupigana katika vita ambavyo havikuwahusu kinaendana na sera za Uingereza juu ya makoloni yake ya Afrika Mashariki na kwingineko. Mhimili wa sera hizi ulikuwa ni kupora raslimali za makoloni pamoja na kuwatumikisha wenyeji kama watumwa. Mambo haya hayaelezwi waziwazi katika riwaya tunayoizungumzia lakini yanadokezwa. Yamkini mtunzi alijikuta katika hali ya

udhibiti ambapo asingeweza kuwashambulia wakoloni moja kwa moja kwa kuhofia kwamba kazi yake isingechapishwa.

Waafrika hawakukubali kuendelea kuishi chini ya utawala wa kikoloni ambapo walifanyiwa maovu yaliyogusiwa hapo juu. Walianzisha harakati za kupigania uhuru wakiwa na ndoto ya kujitawala na kujitegemea kiuchumi. Lakini picha ya dola baada ya uhuru ambayo tunaipata katika riwaya mbalimbali ni ya kusalitiwa kwa ndoto ya uhuru. Matumaini ya maisha bora kwa walio wengi yaliyokuwepo wakati wa kupigania uhuru hayakutimizwa na utawala mpya wa Mwafrika. Sababu mojawapo ya hali hii ni kwamba uhuru uliopatikana ulikuwa wa bandia. Yaani, ukoloni haukung'olewa. Badala yake ulibadilisha sura. Baada ya ukoloni mkongwe enzi ya ukoloni mamboleo ikaingia. Kupitia ukoloni Mambole. Uingereza inaendelea kuyadhibiti kiuchumi mataifa ya Afrika Mashariki ambayo zamani yalikuwa makoloni yake.

Ukoloni mamboleo na madhara yake unasawiriwa katika riwaya ya *Walenisi*. Dzombo ambaye ni kiwakilishi cha walio wengi katika nchi yake anaishi katika hali ya ufukara. Anajitahidi kujitoa katika umaskini lakini anashindwa kwa sababu ya sera mbaya za kilimo zinazofuatwa na nchi yake. Tunaelezwa kwamba nchi hii imeshurutishwa kufuata sera hizi na Benki ya Dunia. Wakulima wanakatazwa kupanda mimea ya chakula na badala yake wanalazimishwa kupanda mimea itakayotoa mazao ya kuuzwa nchi za nje. Benki ya Dunia ni chombo cha mataifa makuu ya kibepari ambacho kinatumiwa kuyadhibiti kiuchumi mataifa maskini. Hapa tunaona kuwa ukoloni mamboleo unaendeleza unyonyaji uleule uliokuwepo katika enzi ya ukoloni mkongwe. Hii ndiyo sababu mataifa ya Afrika Mashariki yameendelea kudidimia katika umaskini hata baada ya uhuru. Tunaona vilevile kuwa vyombo vya dola baada ya uhuru havitumiwi kuwahudumia wananchi na kuboresha maisha yao. Badala yake vinatumiwa kuwagandamiza na kulinda maslahi ya vigogo na mataifa makuu ya kibepari kama vile Uingereza. Kwa mfano, Dzombo anakumbwa na masaibu mengi katika jitihada zake za kujitegemea. Mimea yake inafyekwa kwa sababu upandaji wake unakiuka sera za Benki ya Dunia. Hata anapolima tena na kupanda mimea iliyopendekezwa halipwi kwa mazao yake anapoyapeleka kwenye idara ya serikali inayohusika. Kilele cha kudhulumiwa kwake kinafikiwa anapohukumiwa kifo baada ya kukamatwa na kushtakiwa kwa kusema ukweli kuhusu hali duni ya maisha yake.

Udhalimu wa dola ya baada ya uhuru pia unamulikwa katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Serikali ya Tanzania iliamua kubadilisha mfumo wa kiuchumi na kisiasa kwa kutekeleza sera za ujamaa. Tunapata picha ya jinsi sera hizi zilivyotekelezwa baada ya Azimio la Arusha. Japokuwa sera hizi zilikuwa na

lengo zuri la kuvunja mfumo uliorithiwa kutoka kwa wakoloni na kuanzisha mfumo wenye misingi ya usawa na kujitegemea, utekelezaji wake ulikuwa na udhaifu mwingi. Kwanza, ni wazi kwamba wananchi hawakuhusishwa katika kuzibuni sera zenyewe, na kwa hivyo hawakuzielewa wala kutambua thamani yake. Zilitoka juu kwa viongozi na kuteremshwa kwa wananchi ambao walikuwa na mtindo wao wa maisha na hivyo hawakuzihitaji. Tunaelezwa: "*Hivyo ndivyo wananchi hawa walivyoyazoea maisha haya. Furaha walikuwa nayo na vijiji vya ujamaa waliviona mzigo mzito sana*" (uk.56). Kauli hii inatolewa kuhitimisha maelezo juu ya mtindo wa maisha wa wanakijiji wa Bugolola. Wanakijiji hawakutaka ujamaa lakini serikali ilishikilia kwamba uamuzi wa kutekeleza sera za ujamaa ulikuwa umeshafanyika hivyo hakuna kurudi nyuma. Kwa hivyo, serikali ilitumia mabavu. Tumaini ananyangnywa mashamba yake aliyoyapata kwa njia halali na kwa kufanya kazi kwa bidii. Japokuwa Tumaini pia ana udhaifu wake, lakini ni wazi kwamba anadhulumiwa.

## 3.0 Utamaduni

Tunapata sura mbili za utamaduni katika riwaya tunazohakiki. Kwanza, tunapata picha ya utamaduni wa kiasili wa Kiafrika ambao haukuathiriwa na utamaduni wa Kizungu. Pia, tunapata picha ya utamaduni mseto ambao unatokana na mchanganyiko wa utamaduni wa Kiafrika na ule wa Kizungu. Utamaduni wa kiasili wa Kiafrika tunauona katika sehemu za mashambani ambapo wananchi walio wengi wanaishi. Kupitia masimulizi juu ya kijiji cha Bugolola katika *Dunia Uwanja wa Fujo*, tunaona kuwa wananchi wa mashambani wanaendelea kuishi kama walivyoishi kabla ya majilio ya ukoloni. Wanaendesha ndoa zao kufuatana na mila na desturi za kimapokeo. Wanashiriki katika kilimo cha kiujima katika mashamba ya kiukoo. Wanajiburudisha kwa kucheza ngoma na kunywa pombe ya kiasili. Katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa*, tunapata taswira chanya ya utamaduni wa Kiswahili. Asasi ya ndoa – kama kipengele cha utamaduni huu – imepewa nafasi kubwa katika riwaya hii. Tunaelezwa jinsi ndoa inavyopangwa, kutekelezwa na kudumishwa kwa kufuata mila na desturi za Kiswahili. Tunaona kuwa wazazi wana jukumu la kuwatafutia watoto wao wachumba, kuwashauri kuhusiana na ndoa zao na kushiriki katika kutatua matatizo yanayozuka kati ya mke na mume. Uthabiti wa utamaduni huu unaelekea kutiliwa chumvi tunapoelezwa kwamba hata watoto waliopata elimu ya juu kama Monika wanatafutiwa wachumba na kuozwa na wazazi wao.

Tofauti na Burhani, Kezilahabi anaonyesha kuwa utamaduni wa kiasili wa Kiafrika una mazuri mengi lakini pia una upande mbaya. Kipengele kimojawapo cha ubaya huu ni uchawi. Katika kijiji cha Bugolola tunaona kuwa

watu wengi, wakiwemo wazazi wa Tumaini, wanaangamizwa na uchawi. Mugala, mamake Kasala, anakuja kutambuliwa kuwa ndiye mchawi anayewaroga watu na kuwageuza kuwa vizuu. Mugala anaadhibiwa kwa kuhamishiwa kisiwa cha wachawi lakini hii haimaanishi kuwa uchawi umefutwa kutoka kijijini.

Ubaya mwingine wa utamaduni huu ni ndoa za lazima ambapo wazazi wanawachagulia binti zao wachumba na kuwaoza kwa lazima kwa wanaume wasiowapenda. Mulele anajaribu kumlazimisha bintiye kuolewa na rafiki yake Tembo. Anafanya mipango yote ya kumuoza Anastasia hata anapoonyesha wazi kwamba hampendi Tembo na hataki kuolewa naye. Sababu yake ni kuwa Tembo ni mzee wa miaka 50 huku Anastasia akiwa na umri wa miaka 16. Wazazi wake wanapuuza upinzani wake. Hatimaye analazimika kutoroka na kwenda kuolewa na Tumaini ili kuepukana na ndoa hii ya lazima.

Peter Barry (1995:193) anasema kwamba waandishi wa kibaada-ukoloni huumba taswira mpya ya mataifa yao kutokana na tamaduni za kijadi na kuikataa taswira duni iliyochafuliwa na wakoloni. Kwa kufanya hivi, wanaurudishia hadhi yake utamaduni wa Kiafrika baada ya hadhi hii kuangamizwa na wakoloni. Hivi ndivyo anavyofanya Achebe katika riwaya yake maarufu: *Things Fall Apart*. Hivi ndivyo wanavyofanya Kezilahabi na Burhani katika riwaya tunazohakiki. Ni muhimu kufafanua kwamba kwa kufanya hivyo wakitumia Kiswahili ambacho ni lugha ya Kiafrika, waandishi hawa wanakwenda mbele ya Achebe katika harakati za kuikomboa Afrika kiutamaduni. Mkoloni alijitahidi kuzinyamazisha lugha na tamaduni za Kiafrika. Wanavyofanya waandishi tunaowazungumzia ni kwamba wanazipiga vita jitihada za mkoloni na kuzirudishia sauti na uhai lugha na tamaduni za Kiafrika.

Kezilahabi na Burhani pia wanaangazia utamaduni mseto unaoibuka baada ya ukoloni. Utamaduni huu unajengeka kutokana na mila na desturi za Kiafrika kwa upande mmoja, na elimu ya Kimagharibi na dini ya Kikristo kwa upande mwingine. Dalili mojawapo ya utamaduni mseto katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* ni majina ya wahusika wa kizazi kipya kilichopata elimu ya Kimagharibi na kuathiriwa na dini ya Kikristo. Majina ya kwanza ya karibu wahusika wote ni ya Kizungu. Kwa mfano, watoto wa Kasala na Mungere wanaitwa Dennis, Leonila na Aurelia. Tunaelezwa pia kuwa Tumaini alipobatizwa alipewa jina la Aidan. Rafikiye Tumaini anaitwa John.

Katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa* utamaduni mseto unabainishwa kupitia athari za elimu ya Kimagharibi. Vijana wa kizazi kipya kama vile Rashid, Muna

na Monika wanapata elimu ya juu, wengine hata kutoka ng'ambo. Wanapohitimu, tunawaona wakifanya kazi za kisasa katika idara za serikali na makampuni. Hii inaonesha kuwa elimu ya Kimagharibi ina manufaa kwa vijana kwa sababu inawapa stadi na ujuzi unaowawezesha kufanya kazi. Elimu hii pia inawajengea utamaduni wa kusoma ambao una manufaa makubwa sio kwa vijana tu bali kwa wote.

Lakini utamaduni mseto pia una ubaya wake. Katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa* mhusika mkuu, Monika, anakwenda ng'ambo kusoma na anaporudi anaonekana kuwa mtu tofauti kabisa. Amekengeuka kutokana na elimu na utamaduni wa Uzunguni alikokwenda kusoma. Kutokana na mkengeuko huu anausifu na kuuonea fahari utamaduni wa Kizungu huku akiutweza utamaduni wa jamii yake. Kuhusu Uzunguni anasema: *"Watu wameendelea sana, wana ustaarabu mkubwa. Sisi huku bado tuko nyuma sana"* (uk.146). Monika anashindwa kabisa kupatana na jamaa zake na anaishia kufukuzwa kutoka nyumbani.

Katika *Dunia Uwanja wa Fujo*, ubaya wa utamaduni mseto unabainishwa kwa njia kadhaa. Kwanza, kuna malezi mabaya, pili, kuharibika kitabia kwa baadhi ya vijana waliosoma na tatu, matatizo ya ndoa ya baadhi ya vijana hawa. Mhusika mmojawapo aliyeharibika kitabia ni Tumaini. Kinachochangia kuharibika huku ni malezi yasiyofaa aliyoyapata. Babake, Kapinga ni mwalimu ambaye ana pesa za kutumia kukidhi mahitaji ya familia yake. Lakini, anazitumia pesa zote kumfurahisha Tumaini ambaye ni mtoto wake wa pekee anayempenda sana. Anajitahidi kumlea Kizungu mtoto wake na hatimaye anamharibu. Tumaini anafunzwa kwamba yeye ni mtu wa tabaka la juu na jirani zake kijijini ni watu duni wanaostahili kudharauliwa. Tunaelezwa kuhusu malezi yake: "*Alitafutiwa msichana mdogo wa kumtunza kwa mshahara. Tumaini alikuwa kwa kuengwa. Alinunuliwa vijigari vidogo vingi; kila alicholilia alipewa*" (uk.17). Anapokuwa mkubwa, Tumaini analala ovyo na wasichana kijijini, kuwatia mimba na kuharibu maisha yao. Kwa mfano, anamtia mimba Leonila na kukataa kuwajibika. Anapoulizwa kuhusu kitendo chake anajibu kwa kiburi: "*Mimi siwezi kumuoa Leonila: mimba si yangu. Hata kama akizaa, mtoto wake mnaweza kumtupia mbwa*" (uk. 39). Hata anapooa, Tumaini anaendelea na tabia yake ya kufanya mapenzi ovyoovyo. Tunaelezwa kwamba "*Shauku yake ya wanawake haikupungua. Alikuwa amejizoeza vibaya tangu utoto wake. Ilikuwa vigumu sana kwake kujitawala*" (uk. 103).

Ndoa ya Dennis na Vera, au mama Resi, inatupa mfano mzuri wa athari za uzungu katika utamaduni mseto. Kutokana na elimu ya Kimagharibi walizopata, Dennis na Vera wanaamini kwamba mtindo bora wa uhusiano baina ya mume

na mke ni ule wa Kizungu. Vera anamwambia Tumaini kuwa "*Katika jamii ya Kizungu, utakuta mara nyingi mwanamke ndiye ana sauti zaidi kuliko bwana*" (uk. 104). Kwa kufuata imani hii mume na mke wanafanya mambo ya kuchekesha katika jitihada za kuonyesha kwamba wao ni watu wa kisasa. Kazi za nyumbani kama vile kupika wanafanya kwa zamu kuonesha kwamba wanaamini katika usawa wa kijinsia. Lakini ni wazi kuwa huu ni unafiki mtupu. Mama Resi anayatumia mawazo haya kama kisingizio cha kutowajibika. Tunaelezwa kwamba mtoto wake daima ni mchafu kupindukia kwa sababu anazembea kufanya kazi za nyumbani. Aidha, mama huyu ni mkware anayetumia muda wake mrefu akitafuta vijana wa kufanya mapenzi nao wakati bwanake yuko kazini. Hatimaye ndoa hii inakuja kusambaratika pale Dennis anapogundua siri za maovu ya mkewe na kumtaliki.

## 4.0 Hitimisho

Kwa ujumla, waandishi wa riwaya ya Kiswahili wamezichunguza kwa jicho la kiuhakiki jamii za Afrika Mashariki baada-ukoloni. Wameangazia mifumo ya kiuchumi na kisiasa inayotawala katika jamii hizi. Dola ni kipengele kimojawapo muhimu cha mifumo hii. Ni wazi kwamba dola za baada ya uhuru hazitofautiani sana na zile za utawala wa kikoloni. Hii ni kwa sababu dola hizi zinaendelea kulinda maslahi ya mataifa makuu ya kibepari kama vile Uingereza katika mfumo wa ukoloni mamboleo. Zinaendeleza utabaka na ugandamizaji wa wananchi walio wengi. Kwa upande wa utamaduni, waandishi wanaohusika wanajitahidi kuurudishia hadhi yake utamaduni wa kiasili wa Kiafrika ambao ulitwezwa katika enzi ya ukoloni. Wanaonesha kwamba utamaduni huu unaweza kuwa msingi bora wa utaifa. Wanausawiri pia utamaduni mseto ambao umejengeka kutokana na athari za ukoloni na elimu ya Kimagharibi. Utamaduni huu umekikengeusha kizazi kipya lakini pia umekuja na manufaa, hasa ya kielimu. Mwisho, waandishi hawa wamefaulu kubainisha uchangamano wa jamii za Afrika Mashariki baada ya tukio kuu la majilio ya ukoloni.

## Marejeo

Ashcroft, B. na wenzie (1989). *Postcolonial Studies*, London: Routledge.
Ashcroft, B. na wenzie. (1989). *The Empire Writes Back*, London: Routledge.
Barry, P. (1995). *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory*: Manchester University Press.
Burhani, Z. (1987). *Mwisho wa Kosa*, Nairobi: Longman Kenya Ltd.
*Lugha Juzuu la 1* (1977). Chuo Kikuuu cha Uppsala.
Mbatiah, M. (2003). *Mwongozo wa Walenisi*, Nairobi: Longhorn Publishers.
Mbatiah, M. (1999). "The Origin and Development of the Swahili Thesis Novel in Tanzania" Tasnifu ya Uzamivu: Chuo Kikuu cha Nairobi.
Mkangi, K. (1995). *Walenisi*, Nairobi: East African Educational Publishers.
Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
Robert, S. (1968). *Utubora Mkulima*, Nairobi: Evans Brothers Kenya Ltd.

---

[i] Tazama mahojiano ya Kezilahabi na mwandishi wa Kiswidi aitwaye Bernander katika jarida la *Lugha* juzuu la 1, 1977.

[ii] **Baada-ukoloni** ni istilahi inayotumiwa kurejelea hali ya jamii ambazo ziliwahi kutawaliwa kikoloni, hasa barani Afrika, Asia na kwingineko. Kiini cha hali hii ni athari hasi za ukoloni katika tamaduni za jamii zinazohusika.